

TAARIFA KWA UMMA

UVAAJI BARAKOA

Katika kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inapenda kuwataarifu wadau wake wote na umma kwa ujumla kuwa, **endapo watalazimika kufika katika Ofisi za EWURA**, wavae BARAKOA ili kujikinga na kuwakinga watoa huduma dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona. Yeyote asiyevaa BARAKOA, hataruhusiwa kuingia Ofisini.

EWURA inawashauri wadau wake wote kuendelea kutumia mfumo wa LOIS <https://lois.ewura.go.tz/ewura/> kufanya maombi ya leseni, vibali na kuwasilisha malalamiko kwa njia ya kieletroniki. Wadau wanaweza pia kutumia namba za simu 0800110030 (BURE) na +255-26 2329002-3 pamoja na barua pepe: info@ewura.go.tz kupata huduma mbalimbali.

EWURA inawakumbusha wadau na umma kwa ujumla kuendelea kuzingatia maelekezo ya Serikali kuhusu njia za kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona nchini.

Imetolewa na:
MKURUGENZI MKUU
20 Aprili, 2020